SWAHILI FORUM 29 (2022): 95-113

MANUKATO YA KIMANGA: 'TARABIZUNA' KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI WA KARNE YA 19 NA 20

AHMAD KIPACHA

Uandishi kuhusu ushahidi wa maingiliano katika Bahari ya Hindi katika karne ya 18 na 19 umechukua sura mpya mara baada ya washairi mashuhuri wa Kiswahili kugusia masuala ya utamaduni wa manukato au tarabizuna katika kazi zao. Washairi hao kama vile Liyongo, Mwanakupona, Sikujua, Himidi, Abdalla na wengineo wamegusia suala la manukato kama sehemu ya utamaduni uliokopwa kutoka Asia-Arabuni au Umangani hadi pwani ya Afrika ya Mashariki. Ni kwa nini suala la manukato linatumika kama kigezo cha kuathiriana kitamaduni baina ya Wahindi, Waarabu na Waswahili? Makala haya yanajenga hoja kuwa motifu ya manukato ni mojawapo ya kielelezo cha maingiliano ya kitamaduni baina ya wadau wa Bahari ya Hindi katika kazi hizo za sanaa. Makala yanatoa fursa ya kuliangalia swala la manukato linavyoibua mfumo wa kijamii na suala zima la usawa wa kijinsia, osmolojia, mahusiano ya ndoa, utambulisho na sanaa ya mapambo.

Writing about the evidence of the Western Indian Ocean connections in the eighteenth and nineteenth centuries have taken a new turn following manifestation of the perfumery customs in the works of Liyongo, Mwanakupona, Sikujua, Himidi, Abdalla and others who are classical celebratory Swahili poets and yet they have evoked the perfumery trope in their works as part of the adapted oriental customs in the Swahili coastal littoral. Why is the perfumery trope used as an emblematic entity of influence and contact between Asia, Arabs and African Swahili? This article argues that the motif of perfume in those Swahili poems represents the study of cultural hybridity around the Western Indian Ocean rim. This study gives opportunity for scholars to examine how the perfumery trope symbolizes social issues, osmology (power and marginality), marital relations, identity, and ornamentation customs.

Maneno muhimu: Swahili, poetry, poems, perfume

Utangulizi

Mapambo, manukato, sauti nyororo, na uvutiaji wa mwili wa mhusika Yasmini kwa wanaume wa mbari tofauti huko Unguja katika *Vuta Nkuvute* (Shafi 1999: 31-34) na upambaji na manukato ya majengo, vyumba na mavazi na mwili katika kasri za masultani huko Pate katika *AI-Inkishafi* (Nasir 1972: 75-77) ni mandhari mbili tofauti lakini zenye mahusiano ya kushabihiana. Shafi Adam Shafi na Sayyid Nasir wote wametumia upambaji na manukato ama katika mwili au makazi na mavazi katika kuibua dhamira inayofanana ya athari ya maingiliano ya wanabahari ya Hindi. Utawala wa Sultani uliwezesha kuwepo kwa wahamiaji wa Kiarabu na Kihindi huko Zanzibar katika karne ya 18 akiwemo mhusika Yasmini - mwanamke wa Kiasia. Mapambo ya majengo na watu waliovaa nguo za fahari, *misutu*, na manukato ya kuvutia yatokayo Arabuni yanabainisha athari za utamaduni wa Bahari ya Hindi huko Pate katika pwani ya Kaskazini ya upwa wa

Waswahili kama anavyosimulia Nasir katika *Al-inkishafi*. Kimsingi mapambo ya mwili, nyumba na mavazi yameoanishwa na manukato (uturi, 'tarabizuna'[1]) ambapo fahiwa ya kuona inalandanishwa na fahiwa ya kunusa. Motifu ya manukato katika fasihi na hata tafiti za kiethinografia si jambo geni. Katika hakiki ya Catherine Maxwell ya *Perfume in Victorian Literary Culture* (2017) yenye kupitia ushairi na nathari za waandishi wa mwanzoni mwa karne ya 20 huko Uingereza, kunasawiriwa taswira za manukato, ada za mapambo, wasifu na shajara ambapo tunaona namna mazao ya mimea, wanyama na sayansi ya kikemikali inavyokuzwa katika tasnia ya manukato kiasi kwamba ni vigumu kwa waandishi wa fasihi kukwepa matumizi ya taswira za kunusa kufikisha ujumbe wao. Maxwell anabaini umuhimu wa kuibuka kwa mkondo wa nadharia ya maono na fahiwa hususani inayozingatia unusaji. Kwa njia ya kuvuta pumzi, kupitia mapafu, harufu inatuingia bila kipingamizi. Harufu iwe ya manukato au kutuzi ina uwezo wa kutuvaa katika fikra zetu na kubadilisha hali na mitazamo yetu. Hata hivyo fahiwa ya unusaji haibebeshwi sifa ya kuibua dhamira chanya yenye kuliwaza moyo na kuburudisha macho pekee. Katika andiko la *The Smell of Class* (2001), Janice Carlisle amebaini vilevile kuwa katika fasihi ya Kiviktoria ya Kiingereza manukato yamesababisha wanawake ambao hawakustahiki kuolewa na watu wa tabaka la kati wakaolewa kutokana na kulaghai haiba. Hivyo bado inatiki kuliweka suala la motifu ya manukato katika medani ya majadiliano ya kijamii iwe kwa wema au ubaya.

Katika fasihi ya Kiswahili, hakiki za Mugyabuso Mulokozi (1982), Fikeni Senkoro (1988) na Abdulrahim Taib Ali (2017), zimegusia suala la fahiwa ya kunusa kupitia manukato hususani walipomjadili Mwanakupona binti Mshamu wakati akimuasa binti yake kujipamba na kujisafisha kimwili na kimazingira, pamoja na mume wake na wageni wajao kwake kwa kuhakikisha uvundo, vumba na uchafu haupewi nafasi katika nyumba yake. Senkoro (1988) sambamba na Mulokozi (1982) na Taib (2017) amelitia doa tukio la manukato katika ushairi wa Mwanakupona bini Mshamu na mengineyo yanayofanana kwa hoja kwamba mamwinyi katika *Utendi wa Mwanakupona* (1850) hupendelea:

> [...] sana mambo ya kuvutia macho na kuliwaza pua, kama vile mapambo aina aina, wanawake wazuri, nakshi na marembo ya rangi za kuvutia katika makazi na malazi yao... marashi na manukato, udi na ubani [...] (Senkoro 1988: 6-7).

1 'Manukato' pia hujulikana kama 'tarabizuna' katika msamiati wa Kikae (Chum 1994:43) "Avyokuja manyakani kajitia talabizuna" (alipokuja kichakani alijitia manukato) kuvuta ashki ya mapenzi.

Mhakiki Senkoro hapendezwi na namna ya mapambo ya "kuvutia macho" na "kuliwaza pua". Analinganisha kitendo hicho kama mbinu ya kumdumaza mwanamke kimawazo na hivyo kujihisi yupo kwa ajili ya mwanaume pekee (Senkoro 1988: 6). Wapo walioliona suala hilo hususani linavyojitokeza katika *Utendi wa Mwanakupona* kuwa ni matokeo ya athari ya itikadi za Kiorenti kupitia dini ya Kiislamu na jinsi maandiko ya Korani yanavyoakisiwa katika fikra za mwaandishi ambaye ni muumini wa dini hiyo (Njozi 1990, Taimammy & Swaleh 2013).

Makala hii inazipitia kazi za ushairi wa Kiswahili hususani kuanzia karne ya 19 na 20 na namna motifu ya manukato inavyosawiriwa. Tumeteua *Utendi wa Mwanakupona* (Mulokozi 1999), *Utendi wa Mwanamanga* na *Utumbuizo wa Liyongo Harusini* (Miehe na wenzake, 2006), *Howani Mwana Howani: Tenzi za Zaynab Himid Mohammed* (2004), na *Sauti ya Dhiki* (1973).

Hatahivyo, suala la manukato katika ushairi wa Kiswahili limetamalaki. Kwa upande wa Mathias Mnyampala (2014) anaelezea jinsi nguvu ya maua ilivyo:

> Kuna vitu visodumu ingawaje vyapendeza,
> Huwatia watu hamu, pua moyo huliwaza
> Kama maua matamu, nafsi huyatukuza,
> Uzuriwe huliwaza, kwa macho hata kwa pua (Mnyampala 2014: 59)

Anatutajia aina mbalimbali za maua ya Uswahilini kuanzia *waridi, arafaji, tawiji, nafsiaji, kahawani, barafusaji,* na hata *yasmini.* Tunajenga hoja kuwa tapo la fahiwa ya unusaji katika fasihi (*smelling/odor literature*) limesahauliwa au kupuuzwa katika hakiki za kifasihi ya Kiswahili. Tunaliangalia suala zima la fahiwa ya manukato kwa mtazamo mpana zaidi nasi tu ule wa kuamsha 'ashki' ya mapenzi pekee na utoaji burudani kwa mamwinyi. Makala haya yanakusudia kujenga hoja kuwa manukato na maingiliano ya kitamaduni baina ya wadau wa Bahari ya Hindi ni pande mbili za sarafu moja. Vidokezo vya manukato katika fasihi ya Kiswahili ni sawa na utafiti wa makutano ya kitamaduni katika kazi hizo. Tunatoa mchango wetu sambamba na ombi la Clarrisa Vierke la kuwataka wahakiki waorodheshe ushahidi wa vielelezo vya matini, fikra au mada katika ushairi wa Kiswahili kubaini uhamishaji wa maarifa ndani ya wigo wa Bahari ya Hindi katika katika karne ya 18 na 19. Wito wa Vierke ni kuwa:

> [...] precolonial Swahili texts, most of which are poetry, have hardly been taken into consideration in recent debates on Indian Ocean connections.

> Still one should not forget that there are a number of studies mostly dating back to the beginning of the twentieth century which focused on the historical influence of ideas, motifs, texts and prosodic models coming from Arabic traditions (Vierke 2016: 225-226).

Ni kichocheo kwa wahakiki kutokuzifumbia macho motifu zionekanazo kuwa hazina umuhimu kama vile manukato kama ushahidi wa maingiliano ya kitamaduni baina ya Waorienti na Waswahili katika ujenzi wa utamaduni wa Bahari ya Hindi. Katika kubaini motifu ya manukato sambamba na alama ya uturi au manukato ya Manga, tutaangazia yafuatayo: kuwa tarabizuna ni fahiwa ya kilimwengu, tutatoa ushahidi kuwa manukato ya Kimanga ni motifu katika ushairi wa Kiswahili wa karne ya 19 na 20.

Tarabizuna ni Fahiwa ya Kiulimwengu Haikwepeki

Suala zima la 'utarabizuna' halikwepeki katika ngazi za maisha hadi kifo. Kiuhalisia, mila ya manukato haikuwepo tu katika dola la Kiarabu na Kiasia. Kuanzia dola la Misri, Warumi, Wagiriki, Mesopotamia na baadaye Ulaya nzima ustaarabu wa manukato umetamalaki na kuathiriana (Rimmel 1865, Nigel 1981, Hull 2008, McHugh 2011). Manukato ni taasisi tunayoambatana nayo tangu tunazaliwa, kukuwa, kubaleghe, kuoa au kuolewa, katika maisha ya kila siku na hata siku ya kufa na baada ya kifo. Yapo manukato ya kuondosha udhia wa uvundo au mnuko. Na yapo manukato ya kuamsha hisia na yale ya kujenga siha na utukufu. Miungu ya Misri ya jadi walihesabika kama viumbe vya manukato. Wakinasibishwa na utakatifu. Nerfertum aliitwa "bwana wa manukato" na mungu kijana anayetoa uturi wa ua la "Lotus" (Byl 2012).

Katika Agano la Kale (2 Wafalme 9:30), anaonekana Jezebel akipaka wanja, na hicho kilikuwa kipindi cha miaka 840 KM. Masihi Yesu bin Mariamu alipozaliwa tu, wafalme walimpelekea zawadi ya manukato na vipande vya dhahabu na katika Luka 23:56 tunaonyeshwa kuwa Yesu alipakwa manukato na marashi kabla ya kuzikwa. Waislamu wanakila aina ya manukato, marashi na nyudi (ubani maiti) wanazonyunyiziwa maiti zao kama athari ya utamaduni wa kiorienti. Makahaba wa Kispanishi walijipodoa na poda za rangi ya pinki kuupata ung'aavu na wanawake wa Kitaliano wa karne ya 13 walijipaka rangi za midomo nyekundu, wanja na maskara yenye umaarufu hadi leo. Katika miviga na sanaa za maonyesho za Wachina palitumika aina mbalimbali za mapambo na manukato ikiwemo ubani, mafuta ya wanyama, nta katika kipindi kabla ya milenia ya kwanza (Rimmel 1865).

Katika utafiti wa hivi karibuni wa kiethinografia uliofanyika Zanzibar, Rosabelle Boswell alibainisha kuwa wanawake watu wazima wanawajibika kujipaka mafuta mazuri kama ada ya

kujipodoa na kujisafisha. Na pia wanawajibika kusafisha na kunukisha nguo zao na vitanda vyao kwa kutumia uturi kama ule wa udi, asmini na marashi (Boswell 2008:301). Amour Khamis (2008) sawa na Boswell (2008), anasema kuwa wanawake wa Kizanzibari hujipamba kwa 'vyombo vya dhahabu, fedha au kareti kama bangili, vidani, vipini, pete na herine. Aidha hutengeneza vikuba na mapambo mengine kwa kutumia maua yanayonukia kama mkadi, asumini, viluwa au mawaridi' (Khamis 2008: 11). Mbali ya mapambo ya kunukia, na vito vya kung'aa wanavyovaa wanawake, pia hujifukiza, kujipaka na kujipuliza manukato ya aina mbalimbali kama vile 'podari, mafuta mazuri ya haliudi, tarabizuna, na miski' (Khamis: Keshatajwa). Khamis na Boswell wanaweka wazi kuwa tabia ya manukato kwa wanawake hujitokeza pale wanapokuwa nyumbani, wanapokwenda harusini, safari ya matembezi au hata kazini. Wote wanatugusia pia kwamba baadhi ya wanaume husingwa na wanawake zao kwa mafuta ya karafuu au dawa za kienyeji ili kutakatisha miili yao. Hata hivyo kupitia kazi za Boswell (2008) na Khamis (2008) hatuelezwi kwa kina ni mambo gani ambayo mwanaume naye anamfanyie mkewe katika kutimiza wajibu wake kama mpenzi mwenza. Hii labda ni sehemu ya utafiti inayongoja kutafitiwa zaidi.

Kwa upande wa jamii ya Waswahili, je, kuna ushahidi wowote ule unaothibitisha kuwa kidesturi Waswahili wanautambua mchango wa manukato katika maisha yao kiujumla? Swali hili linajibiwa na uwepo wa methali ya Kiswahili isemayo kuwa "Mfuatana na Mmanga hunukato" (Wamitila 2004: 207). Methali hii inaikumbusha hadhira mojawapo ya athari ya maingiliano kati ya Waorienti na Waswahili. Watumwa waliokuwa wakisafiri pamoja na Wamanga walisikia aina ya harufu ya manukato. Wake walioolewa na Waarabu walinukishwa manukato mapya wakayachukua kama sehemu yao ya maisha. Kuja kwa dini ya Kiislamu nako kuliibua utamaduni wa ubani na marashi unaohimizwa kama sehemu ya usafi. William Hichens (1938: 75) anathibitisha kuwa Waswahili walikopa tabia ya kujifukiza na kujipaka manukato ya marashi na uturi katika miili, nguo na hata vitanda vyao kama wafanyavyo waarabu wa Bahrain na Shirazi na India.

Msisitizo wa aina ya uturi utokao Umangani unaotumiwa na Waswahili unajitokeza zaidi katika kazi za fasihi kama tutakavyothibitisha katika makala haya. Manukato na Umanga au Manukato ya Kimanga yanapewa msititizo wa pekee pale inapozungumziwa fahiwa ya harufu kama nyenzo muhimu ya kisitiari kwa wasanii wetu. Ukanda wa Manga unajumuisha nchi na miji ya Omani, Maskati, Dhoha, na Yemen, Aden, Hadramawt na Sokotra (Nicolini 2003, Adam 2015). Kyallo Wamitila (2004: 167) ameifasiri dhana ya 'Manga' kumaanisha "neno ambalo linatumiwa kwa maana ya Uarabuni na anasema linapatikana sana katika tungo za ushairi." Tunathibitisha hayo kwani katika utenzi wa liyongo wa "Swifa ya Mwana Manga" ingawa unafasiriwa kuwa ni utenzi

wa Liyongo anaomsifu mkewe tangu nywele hadi unyayo, jina la 'Mwana Manga' linajitokeza (angalia Mulokozi 1999: 3 na Mdungi 2009: 61).

Washairi wa Kiswahili nao wamejinaki na lakabu ya 'Mmanga'. Wakati wa kumnasihi asichukue hatua ya kuwajibu wapinzi wa ndoa kishairi, mwalimu wake wa ushairi Mahmoud Hamdouniy au "Jitu-kali", mshairi Khamis Amani Nyamaume (1926-1971) katika *Diwani ya Ustadh Nyamaume* (2004: 12) katika shairi lake la "Taa ya Ndoa" anamwita jitu kali kwa lakabu ya 'bingwa wa Kimanga'. Na hata ushahidi unapatikana katika *Utenzi wa Vita vya Wadachi* bwana Zahoro bin Suwedi aliyekuwa mwarabu aliyejaribu kuonyesha upinzani dhidi ya Wajerumani huko Pangani aliitwa kwa lakabu ya 'Zahoro mwana wa Manga' kumaanisha Zahoro mwenye nasaba na Uarabuni-Oman (Hemedi 1891). Swala kuu katika hakiki zetu ni kubaini kwa kina kwa nini uturi wa Kimanga unasisitizwa na washairi wetu mashuhuri?

Tunajenga hoja kuwa kitendo cha Waswahili kubaini aina ya manukato kuwa ni Umangani kina nia ya kuiweka kumbukumbu ya historia ya maingiliano ya kitamaduni na athari zake. Katika kuingiliana kumekuwepo na athari nyingi za Waorienti katika upwa wa Uswahilini ikiwemo athari za muziki wa taarabu (Eisenberg 2017), visaasili (Knappert 1979), falsafa (Kresse 2009), mapishi (Amidu 2009), ukopaji wa misamiati ya Kiorienti (Lodhi 2000) na utanzu wa ushairi (Vieke 2016). Je, motifu ya manukato ya Kimanga inaakisiwaje katika ushairi wa Kiswahili?

Manukato ya Kimanga ni motifu katika Ushairi wa Kiswahili wa karne ya 19 na 20

Washairi wajadi na wamapokeo wa jinsia zote wamegusia ishara za manukato katika kazi zao. Mwanakupona bini Mshamu (1810-1860) aliyezaliwa Pate, alimtungia bintiye Hashima Mataka (1841-1933) utendi maarufu wa *Utendi wa Mwanakupona* (1858) katika kipindi cha utawala wa Omani (1730-1890). Aliutumia utenzi huo kumuasa binti yake maisha yenye kudumisha mahaba katika ndoa na mumewe. Ni utendi ambao kwa kizazi cha leo unaingia katika mafundisho ya unyago au nyiso. Fumo Liyongo (1160-1204 kwa makadirio tu), mshairi wa Pate alitunga tendi mbili zenye kumakinikia manukato ya Kimanga pale alipotunga 'Utendi wa Mwanamanga' na 'Utumbuizo wa Liyongo Harusini' (katika Miehe na wenzake 2006). Zaynab Himidi (1918-) katika utenzi wake *Howani Mwana Howani: Tenzi za Zaynab Himid Mohammed* (2004) aliwatungia binti zake na wanawake wa Wauswahilini kwa ujumla ada za kujitunza kuanzia utoto hadi utuuzima, katika kipindi cha ukoloni wa Kiingereza na Kiomani na hata baada ya mapinduzi ya 1964. Si washairi hao pekee waliojitokeza kusawiri manukato ya kimanga, wengineo ni akina Mwalimu Sikujuwa bin Abdalla Batawi (1810-1889), Abdilatif Abdalla (1946-), pamoja na kundi la

warasimu wapya kama Shaaban Robert (1909-1962), Mathias Mnyampala (1917-1969) na Kaluta Amri Abeid (1924-1964).

Katika *Utendi wa Mwanakupona* (1858), jukumu analopewa mwari ambaye ni binti yake Mwanakupona ni kuwa ahakikishe anamtunza mume wake kwa kumnyoa, na kumfukiza *udi*:

> Mnyoe mpalilize
> Sharafa umtengeze
> Na *udi* umfukize
> Bukurata wa ashia
> (Mulokozi 1999: 128).

Hapa anafundwa juu ya wajibu wake kwa mume wake. Pia anafundwa namna ya yeye mwenyewe kuhakikisha anakuwa katika kiwango cha juu cha usafi kwa kujisinga na kuweka kikuba cha asumini kichwani na kitandani (firashani) na pia kujinyunyuzia marashi na kujifusha mwili wake ili kunukia.

> 38.
> Na kowa na kuisinga
> Na nyee zako kufunga
> Na asmin kutunga
> Na firashini kutia
>
> 40.
> Na kidani na kifungo
> Sitoe katika shingo
> Mwili siwate mwingo
> Kwa marashi na dalia

Ulimwengu wa Mwanakupona unaashiria taratibu na ada za Waswahili katika kumuandaa mwari. Mafunzo hayo yanazungukwa na tarabizuna za Kimanga zenye kutokana na athari ya muingiliano wa kitamaduni wa Waorienti na Waswahili.

MANUKATO YA KIMANGA: 'TARABIZUNA' KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI WA KARNE YA 19 NA 20

Katika "Utumbuizo wa Liyongo Harusini" katika andiko la Gudrun Miehe na wenziwe, tunamwona Lyongo anasifia nguo (zisutu) za harusini za Waswahili kama vile nguo za Hariri, na "Fedhati na k'owa za Hindi" na "mikufu ya kwawiya shingi". Kwa upande wa manukato anatunusisha "ungi wa mwingo" (uturi mwingi) na "choshi na maambari na udi", pachori na zafarani na twahara ya fungo na itiri na kafuri:

Kuna gungu nyemi za harusi, humuoza umbule Liyongo
P'indi sizo watu wasiyakaa, ukumbini kukawa kisongo
Na muchendavaani libasi, mujifishe na ungi wa mwingo
Mujipake na twibu hiyari, yalotuwa kwa zema ziungo
Choshi na maambari na udi fukizani nguo ziso ongo
Fukizani nguo za Hariri, na zisutu zisizo zitango
Pachori na *zafarani*, na *zabadi* twahra ya fungo.
(Miehe na wenziwe 2006: 40-41)

Aina mbalimbali za manukato na mafusho kutoka Arabuni na kwingineko kama China na India ambako nguo za hariri hufumwa zinabainishwa katika ushairi wa Fumo Lyongo. Katika kuwaita wenziwe wachezao ngoma na kuimba, Lyongo anawataka wanawake wajifukize *maambari* na *udi* katika nguo zao za hariri. Wajipake mwilini zafarani, zabadi na karafuu. Na pia anawashauri wanaume kuwatwaa "wari wa mapambo wa sauti njema ya muango" wajipakao manukato ya *ambari* na kafuri. Lyongo anabaini waziwazi juu ya kuwepo kwa manukato kutoka umangani pale anapomsifu mpenzi wake amwitaye Yanga au Mwanamanga katika ushairi wake ulionukuliwa na katika Miehe na wenziwe (2006: 60-61). Shairi hilo inasemekana alilitunga mwaka 1517. Anataja waziwazi namna ya kwapa, midomo na hata 'farji' ya mkewe inavyotoa harufu nzuri ya manukato ya Kimanga. Kwa mfano kwapa zake:

Hutoa harufu zaidi ya kafu
Au manukato mafuta ya manga (beti 12-31)

Kwa hiyo kuanzia karne ya 14 tayari Waswahili au Washairi wa upwa wa Kiswahili walishapata manukato ya aina ya mafuta kutoka Manga. Isitoshe pia anatueleza juu ya kitovu cha mpenzi wake amwitaye Mwanamanga kuwa '*Kitovu ni huka kezo la kimaka, Mwenye kukinuk'a puwa damu*

henga' (beti 12-38). Na haishii hapo tu anatuingiza chumbani kwake wakati wa kujamiiana na mkewe na bila haya anatudokeza kuwa baada ya kufika 'kileleni', tunda la mkewe lilimlewesha na kumpagaza kwa harufu nzuri ya manukato ya kimanga: *Ikimikamika ikinuk'anuka vumba la kimaka yakwe Mwana Manga* (beti 12-47) na hakuwa na la kufanya ila kuomba tiba kwa waganguzi wa maruhani. Penzi la mkewe linamrusha akili na kumpoteza fahamu, na kikubwa zaidi ni harufu ya penzi lake linavyowehusha. Kupitia Lyongo tunathibitishiwa kuwepo kwa umaarufu wa mafuta ya tarabizuna au manukato, wanja na nguo za kiManga.

Washairi wanatutanabaisha kuwa mapambo, nyudi na wanja bora zinanasibishwa na Umangani[2]. Mwalimu Sikujua akimsifia mtumwa wake (mkewe) amwitae Sihaba anamvalisha nguo (libasi) za uMangani:

> Nimpambe tume wangu, kwa libasi za *Mangani*
> Nguo za kae na tangu, zenye kima na thamani
> Nilifunuwe *tawangu*[3], nitie chema kidani
> Atie mwake shingoni, afurahike sihaba (Chiraghdin 1987: 70)

Na baada ya kuvaa nguo za umangani, mtindo wa kujipamba kama ule wa kujitinda kope, na kupaka wanja unasibu uendane na ule wa Kimanga (Kiarabu). Mara baada ya kuoga ili aweze kuvutia (zaini) na apitapo apendeze machoni.

> Asemende na ghadhabu, kwana enende chooni
> Ndiyo avae *thiyabu*[4] na khulia za thamani,
> Ajisonge *kiarabu, ajitinde* na sikini
> Na *wanda* uwe matoni, ajizaini sihaba (Chiraghdin 1987: 70)

Kwa Sikujua manukato ya kiwango cha juu katika jamii ya Waswahili ni yale yatokeayo "Umangani" kwa enzi hizo na hata hivi sasa:

---

[2] Utamaduni wa Kimanga umetamalaki katika desturi za Uswahilini. Waswahili wanabaini wazi maeneo kama vile Mangapwani, matunda kama komamanga, viungo kama pilipili manga na kungumanga, wanja wa Manga, n.k. (angalia Kipacha 2015: 214)

3 Tawangu ni 'kasha la kizamani' (Chiraghdin 1987: 105).

4 Thiyabu ni 'nguo' (Chiraghdin 1987: 105).

Upatezidi komashi uwe '*atari za Manga*[5]
Ikondoke tashiwishi, wende kwa kujelelenga
Ujuwe si wa ubishi, mwenyewe ukijenga
Wenye kuvua maninga[6], wafurahike sihaba
(Chiraghdin 1987: 70)

Huo uturi maalumu wa Manga utokanao na *waridi, haliudi, misiki, yasimini, mkadi, muafu* na hata '*liwandari'*[7] unasemekana kuwa na nguvu za kupoza maradhi ya mwili na moyo. Maradhi ya moyo yako ya aina nyingi ikiwemo vurugu za maono na kukosa ashki. Sikujuwa anayapamba mapambo na uturi utokao Manga (Uarabuni) kuwa yana nguvu za kuondoa maradhi ya maono na huamsha ashki, na upweke unaowasumbua wanajamii yake hususani wanaume:

Mwenye ndwele yuapowa, kwa ua[8] hilo la *Manga*
Akapata na afuwa , kwa mola wetu wa anga,
Humwisha mtu ukiwa, ajapokuwa muwinga
Ambae yawalienga, hwisha huzuni sihaba
(Chiraghdin 1987: 70)

Nae Abdilatif Abdalla, huku akiwa gerezani, analijiwaza baada ya msongo mkubwa wa mawazo ya kuwekwa kifungoni bila ya hatia. Kinachomliwaza katika madhila yake ni kile anachotuchorea katika *Sauti ya Dhiki* (1973) ambapo mwanamke aliyejinyoosha kitandani huku kapunguza mwali wa taa na kipepeo mkononi anampa liwazo katika hali ya misukosuko. Mtunzi anatunukisha uturi wake na nyudi kutoka Uarabuni:

Manukato muwilini, vyema yalifukizika
Ni *nyudi za Arabuni*, ambari na kadhalika
Ambao wavibaini, wajuwa vinavyonuka

---

5 Atari za Manga ni 'Manukato ya Uarabuni' (Chiraghdin 1987: 105).
6 Maninga ni 'wenye macho au waonao' (Chiraghdin 1987: 105).
7 Liwandari ni 'aina ya manukato' (Chiraghdin 1987: 105).
8 Mshairi Ali bin Said bin Rashid Jahdhmy (Kamange) 1830-1910, aliyeishi Pemba anatuchorea mwanamke anayemfananisha na tunda la "pera" ambaye amemchota akili yake kabisa: Ni yeye sina wa pili, amma yake ni ibura / Umshikapo muwili, huruka kama mpira! / Khaswa ukimkabili, humuoneya khasara, / Rabbi amenipa pera, tunda jema la Peponi. (Abdalla 2016: 38)

Msojuwa ulizani, kwa ambao vyatumika
(Abdalla 1973: 103)

Haishii katika nyudi za Arabuni bali anakwenda mbali zaidi katika shairi la 'kutendana', ambapo Abdalla anaunda majibizano baina ya Mwanamume na Mwanamke, anaupa sifa ya pekee wanja wa kiManga ambao anasema una sifa ya kiwango cha juu ingawaje mdomoni huyo mpenzi wake ametumia rangi ya mdaa ya asilia na siyo itokayo Ulaya.

Na humo mwake matoni, ni wanda ameupaka
Ule wanda wa *Mangani*, mno unaosifika
Namo mwaka midomoni, wekundu unzunguka
Si warangi ulayani, ni mdaa kutumika.
(Abdalla 1973: 89)

Kwa kubainisha uwezekano wa kuwa na bidhaa za Umangani, Ulaya na asilia katika milki ya Mswahili, mtunzi anatupa picha ya kuwa Waswahili wanabainisha ubora wa bidhaa wazitumiazo. Si kila kitu kitokacho nje cha mapambo na manukato basi hukipapatia, huchagua kile kilicho bora. Kihistoria, tunarudishwa katika uwanda wa kijiografia uliosambaa baina ya Bahari ya Hindi Magharibi na Upwa wa Waswahili ambapo kupitia pepo za Monsuni za Kaskazi–Kusi waliunganishwa watu kutokea Peninsula ya Uarabu na Ghuba ya Uajemi wakifanya biashara ya bidhaa za pembe, watumwa, vito, shanga, vyombo, nguo, ubani (manukato) na wenyeji wa upwa Waswahili tangu Karne ya 2 BK (Lodhi 2000, Nicolini 2003, Boswell 2008, Adam 2015). Kisanaajadiya, Waorienti na Waswahili waliathiriana kilugha na kifasihi ambapo ushahidi umebaki katika hazina ya masimulizi yenye athari za Kiarabu na Kiorienti kama Sindbadi Baharia na Abunuwas.

Kiuchumi tunadokezwa na mshairi Muyaka wa Muhaji (1776-1840) wa Mombasa kuwa yeye kama mfanyabiashara alikuwa akisafirisha bidhaa kwa majahazi "kwenda miji mbalimbali ya pwani kama vile Ngazija, Bukini, Unguja, na vilevile kwenda katika miji ya Arabuni na hata Bara Hindi" (Chiraghdin 1987: 6-7). Hayo anatudokeza mwenyewe katika shairi lake la "Baada ya Dhiki Faraji":

Kwaheri mwana kwaheri, nenda zangu Ngezimaji
Nimeazimu safari, kwa pepo za maleleji
Kwa mlenge na shuwari, natawakali Mpaji

Baada dhiki faraji, hakuna lisilokuwa.

Bila ya shaka mshairi kama huyu ameathiri na ameathirika na tamaduni mbalimbali za sehemu alizotembelea wakati wa biashara na kuna uwezekano wa kujishughulisha na biashara za bidhaa za manukato au atari za Manga kama vile ubani, udi, ambari, zinduna, karafuu, marashi, kafuri, wanja n.k) baina ya nchi za ukanda wa bahari ya hindi magharibi hadi upwa wa Uswahilini tangu Karne ya 2 BK.

Matokeo ya maingiliano ya Waorienti na Waswahili yalijenga mseto wa utamaduni hususani katika lugha, fasihi, muziki na visasili vya Waorienti. Muathiriano wa kitamaduni baina ya Waorienti na Waswahili upo katika ngazi za kidhahania na kimaada; Kidhahania ni muathiriano wa kidini, kifalsafa, kiitikadi na kisheria (Pouwels 1987, Rettova 2010, Verne 2012, Vieke 2015) na kwa upande wa muathiriano wa kimaada ni ule wa kitekinolojia, kiusanifu majengo, mavazi, kilimo na chakula (Horton & Middleton 2000, Massamba 2017). Katika sehemu ya kilimo na chakula kuna kundi dogo la athari ya bidhaa za manukato ambalo halijapewa fursa ya kujadiliwa kwa kina na ndio kiini cha makala haya.

Uhusiano kati ya fahiwa ya harufu na wanawake katika ushairi

Katika mjadala wa *Utenzi wa Mwana Kupona* wa Mwanakupona Bini Mshamu (1790-1860), wahakiki Mulokozi, Khatib, Senkoro na Taib Ali wameupa utenzi huo majukumu matatu; kwanza ni wa kumfunza binti aliyeolewa majukumu yake kwa mume wake. Pili ni ushauri wa jinsi mwanamke anayowajibika kujiweka katika hali ya usafi na tatu ni tabia njema kwa mume wake hususani imani ya maisha ya siku ya ufufuo. Moja ya ada ya unyagoni ambayo Mwanakupona anamfunza binti yake ni namna ya kumsinga mumewe kwa manukato na yeye pia kujiweka katika hali ya usafi na kuvutia kwa "asimini kutunga, kwa uwezalo mbuji/ Na firishani kutia, angusa kumtendeya" (mume) (Chiraghdin 1987: 39). Mulokozi anabainisha majukumu ambayo Mwanakupona anamuajibisha mke kwa mumewe kuwa ni:

> [...] kumpa kila analolitaka, kumuaga vizuri anapotoka na kumpokea kwa furaha anaporejea, kumpapasa na kumpepea usiku, kumkanda mwili, kumtukuza na kumsifia kwa watu, kumwandikia chakula, kumnyoa ndevu na kumfukiza udi, na kufanya mazingira yake yawe safi (Mulokozi 1999: 108).

Kitendo cha kumfukiza udi na kuyafanya mazingira ya mume kuwa safi kinabainishwa na washairi wa Kiswahili akina Mwanakupona Mshamu, Fumo Lyongo, Abdilatif Abdalla, Zaynabi Himid, na

Mwalimu Sikujua. Washairi hao wanawapa wanawake uwakala wa kusambaza harufu nzuri ya waridi, asumini, ambari, na mkadi ili kupenya katika mapafu ya wanusaji na kujenga rihi nzuri. Katika *Sauti ya Dhiki*, Abdilatif Abdalla anamsawiri mwanamke anapovaa kikuba cha asumini na waridi kuwa anasambaza fahiwa tatu za kuona, kunusa na kisha hupelekea uamshaji wa hisia ya ugusaji:

> Kimitizama kitwani nyele zilivyotanika
> Usitizame na pini jinsi alivyotomeka
> Na shada la asumini, alivyo kulipatika
> Lazima utatamani, ngaa upate zishika
> (Abdalla 1973: 103)

Anapoangalia nywele na kikuba cha asumini, kupitia fahiwa ya kuona, pua zake zikinusishwa harufu nzuri ya asumini, anakuwa anaishiwa nguvu kiasi cha kuamshwa ari ya kumshika mpenzi wake. Liyongo naye aliponusishwa kapwa za mkewe alipagawa na kupandisha maruhani kwa harufu aliyoiita '*vumba la kimaka'*, afu au 'matukufu mafuta ya Manga' (Miehe na wenziwe 2006: 60-62). Amri Andanenga katika kuelezea kero yake juu ya uwezekano wakuwepo kwa mapenzi yenye adha baina yake na mpenzi wake anayemwita 'mrembo' anatumia sitiari ya kunusa kukemea 'mapenzi ya shombo' katika shairi lake la 'Fanya Ulizio' (1993:89).

> Leo nina jambo, nataka kwambia
> Sikize mrembo, badili tabia,
> Mapenzi ya *shombo* sitavumilia
> Nataka mapambo, sitaki udhia
> (Andanenga 1993: 89)

Andanenga anaitumia fahiwa ya kuonekana kwa macho pale anapomtaja mpenzi wake kwa sifa ya 'mrembo' na penzi la 'kumeta'. Anagusia zaidi kuwa mbali ya kuonekana au kumeta kwa macho anadai kuwa 'mapenzi ni ladha'. Ladha inagusia fahiwa ya kuonja kwa ulimi kama sehemu ya ukamilifu wa mapenzi baina ya wapendanao. Na katika kuangazia fahiwa ya kushika, Andanenga anakerwa na tabia ya mrembo wake kuwa na wanaume 'wengi kuambata' badala ya yeye peke yake. Kimsingi hoja yake ni kuwa anachukia hali ya kuwa na mpenzi wake mwenye tabia mbaya

na mwenye ukosefu wa staha. Katika kuwafikishia wasomaji wake uzito wa kero hiyo anaigeukia fahiwa ya kunusa kwa kutumia sitiari ya 'mapenzi ya shombo' ili kulifafanua suala la aina ya mapenzi yanayomchukiza. Anajenga hoja kuwa unaweza kuwa na mpenzi 'mrembo' na mwenye 'ladha' nzuri lakini ndani yake akiwa na sifa ya shombo, sifa anayoijengea sitiari ya harufu mbaya. Matumizi ya sitiari ya kunusa (smell/olfactory metaphor) kama alivyogusia Andanenga katika shairi lake yanatoa fursa pana zaidi katika fasihi ya Kiswahili kujadili nafasi ya sitiari ya kunusa dhidi ya kushika na kusikia katika uono ulimwengu wa washairi wa Kiswahili. Sitiari hiyo inaweza kutumika katika mifumo jamii mbalimbali kukidhi matakwa ya matabaka husika.

Washairi wa kiume na wakike kama Andanenga, Robert, Mwanakupona na Himidi hawataki kabisa mabinti au wapenzi wao kunuka shombo. Mwanakupona anamkanya bintiye kuwa 'muili siwate mwengo' (Mulokozi 1999: 129). Kwa Zaynab Himidi katika Yahaya & Yahaya (2004: 46) naye anaonyesha wajibu wa ndani wa kumtendea mume, kumwandalia chakula na hata kumlisha na kumpangusa mikono. Ili kukamilisha usafi na mahaba 'Hampaka haliudi / Anukie makusudi'. Kwani hataki akumbwe na 'Harufu vumba hasidi' (Yahya & Yahaya, 2004:46). Kitendo cha kufananisha vumba, shombo na harufu mbaya na uhasidi kinatafsirika kuwa, harufu mbaya huchukuliwa kuwa ni sawa na maradhi, nuksi, ubaya, dhambi, uibilisi, na kila kilicho hasi. Kwa mantiki hiyohiyo harufu nzuri huchukuliwa kuwa ni umalaika, utukufu, nuru, uangaza, rehema na kila sifa chanya ya mwanadamu. Usafi wa harufu nzuri ni msingi wa ucha-Mungu kwa wenye imani za kidini (Byl 2012, Arslan 2019).

Harufu ya kimazingira ina nguvu ya kubadilisha tabia za watu. Ina uwezo wa kubadilisha roho ya ndani na kubadilisha tabia ya mtu. Kwa ajili ya kusafisha fahiwa. Lakini si tu kwamba wanawari walifunzwa juu ya kumtunza mume pekee, manukato ni dawa katika *Howani Mwana Howani* ambapo waja wazito hufushwa kwa "mivuje" na "habasodi chetezoni' ili kuwandaa kwa kujifungua (keshatajwa: 4). Na mtoto akizaliwa hupakwa 'wanja' machoni na nyusini 'Kijuso hachonekani' kumwepusha na jicho la husuda (keshatajwa: 5). Takrima ya kupakwa udi na marashi na kufukizwa ubani hufanyiwa wageni 'Haluidi kupakiwa, Huma mwao mikononi' (Ishatajwa: 57) pale wanapotembelea majumbani na kupewa chakula. Kitendo hicho cha kuwafanya wanukie wanapomaliza kula kinafanyika ili wasiondoke na shombo haswa la samaki, na ni kitendo kinachoshauriwa kiafya kwa mujibu wa nadharia za *kimiasma*[9].

9 Kwa mujibu wa nadharia ya kimiasma ya kinga dhidi ya maradhi, au nadharia ya "harufu mbaya', uchafu wa harufu mbaya unaweza kusababisha maradhi. Muasisi wake Florence Nightingale (1820-1910) aliamini juu ya kuweka mazingira ya hospitali masafi, na yenye hewa nzuri.

Mwanakupona na Zaynab kupitia ushairi wanajivika ‘ukungwi’ na kuzungumza na “wari” wao. Hivyo muktadha wa wari umeletwa kwetu wasomaji na sisi kupitia mwegamo wa mwitikio wa usomaji na sisi tunatoa hukumu zetu. Tukiyachunguza mazingira ya Shaaban Robert katika “Hati” anavyozungumza na binti yake tutakuta lugha na staha anayoitumia ni ile ya baba na binti yake. Lugha yake ina mipaka inapofika katika suala zima la manukato. Shaaban Robert (1972:11) si “nyakanga” ni baba hivyo kuna mipaka ya kujieleza kwa binti yake. Katika *Almasi za Afrika* anatujengea picha ya koja la maua katika shairi la “Koja Hili” linavyojinsishwa kwa kuvaliwa na wanawake pekee kichwani.

Koja jema kwa mtungo, wa mashada maridhawa
Yanayonukia *mwengo, marashi na uturia*,
Yatoke juu ya kingo za mito yanakomaa
Yametungwa mviringo, kojani yaningima
Kweli kitu cha maringo kwa wenye kuitumia (Robert 1972: 22)

Na si kila wakati washairi hujishughulisha na uturi wa hapa duniani. Kwa imani ya Sarahani bin Matwar (1841-1926) mshairi wa Pondayani Pemba anaihama dunia na kufika katika bustani ya peponi ambako:

Huisikiya kwa mbali, rihi miski na udi
Uturi *minal-ali*[10], ambazo si maujudi
Na *mishmishi*[11] fadhali, asmini na waridi
Ramadhanil-imadi[12], jama nimehamiya
(Abdalla, 2016: 88).

Kufuatana na itikadi yake, Sarahani bin Matwar anaiwazia pepo yenye rihi nzuri na maua ya asumini na waridi ya kupendeza anayotarajia kuhamiya. Pengine alikuwa katika siku zake za mwisho na alijitabiria kifo chake na safari yake maisha anayotarajia kuishia. Na katika nchi zenye mapenzi bora, Shaaban Robert amezipamba kwa sitiari ya manukato ya kunukia yenye ‘miski na

10 Minal-ali ni “manukato ya hali au kiwango cha juu”.
11 Mishmishi ni “aina za maua”.
12 Ramadhanil-imadi ni nyumba kubwa (pengine ni ya peponi).

ambari' na ilhali dunia ya mchafukoge ameipaka 'kutuzi'. Miski na ambari ni vielelezo vya tarabizuna za umangani zilizokubalika katika mazungumzo na mijadala ya kijamii kama sehemu ya utamaduni wa Waswahili.

Hitimisho

Makutano ya Waswahili na 'Mwamwinyi wa Kiarabu' yamesababisha kuambukizwa kwa desturi ya manukato ya kuvutia macho na kuliwaza pua kama vile marashi, udi na ubani. Makala haya yametoa mchango wa kuitizama fahiwa ya kunusa kwa jicho pevu. Kupitia motifu ya tarabizuna suala la fahiwa ya unusaji halikwepeki katika tawala na nyakati zote. Kubwa mno katika makala haya ni kuitumia motifu ya fahiwa ya unusaji kama ushahidi mmojawapo wa athari ya maingiliano baina ya Waorienti na Waswahili katika muktadha wa bahari ya Hindi magharibi kama alivyodai Clarissa Verke (2016). Ushairi umebaini kuwa kiungo cha Umanga ni cha kihistoria. Kutamaliki kwa msimbo wa 'Umanga' unaoanishwa na manukato na mapambo ni ushahidi tosha. Suala la mapambo na manukato ni zaidi ya maua na uturi. Mtazamo wa Mwalimu Sikujuwa (1810-1889) unatuweka wazi kuwa tuzame zaidi ya maumbo ya nje ya manukato:

> Ni ua la tamaduni, msambe ni la muafu
> Si waridi si ramani, si huo mtunda ufu
> Hilo halipatikani, hata kwa mia alifu
> Mkiwa wazingatifu, zingatiani sihaba
> (Chiraghdin 1987: 73).

Suala la manukato ni kipande kidogo kinachoashiria pande kubwa la barafu lililomo chini ya bahari linalohusu utamaduni kwa mapana yake. Dokezo la methali ya "Mfuatana na Mmanga hunukato" ni kiashirio cha historia ya makutano na kuathiriana baina ya Waorienti na Waswahili na namna Waswahili walivyoafiki kuingiza katika utamaduni wao desturi ya manukato ya Kimanga. Ombi la Vierke la kuwataka watafiti kubainisha matini, mawazo na viashiria vya kimaada ambavyo vinagusia kuwepo kwa mtagusano na athari baina ya Waorienti na Waswahili katika kile akionacho kama utamaduni wa bahari ya hindi magharibi bado liko wazi. Haja yake ni kuwa pawekwe wazi athari za maingiliano hayo kupitia ushairi baada ya kazi mujarabu za wanaisimu, wanaethinografia,

wanafalsafa na wanahistoria kutekeleza wajibu wao (Lodhi 2000, Boswell 2008, Amidu 2009 na Kresse 2009).

Marejeo

Abdalla, Abdilatif (Mh.). 2016. *Kale ya Washairi wa Pemba Kamange na Sarahani*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Abdalla, Abdilatif. 1973. *Sauti ya Dhiki*. Dar es Salaam: DUP.

Abdalah Hemedi. 1891. *Utenzi wa Vita vya Wadachi.* Dar es Salaam: Education Services Centre Ltd.

Adam, Michel (Mh). 2015. *India Africa: Minorities of Indian Pakistani origin in Eastern Africa*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Amidu Assibi. 2009. A Note on a Shared Heritage: The Bread Culture of the Waswahili of Zanzibar. *Journal of Humanities (JH)* 1,1: 1-11.

Andanenga Amiri. 1993. *Diwani ya Ustadh Andanenga.* Peramiho: Benedictine Publications Ndanda.

Arslan Kalay. 2019. A Heritage Reflecting The Elegant Culture of The Ottoman Empire; Censer and Rosewater Sprinkler Specimens in Bitlis Ethnography Museum. *Journal of History Culture and Art Research,* 8,2: 154-169.

Byl, Sheila-Ann. 2012. The Essence and Use of Perfume in Ancient Egypt. MA at University of South of Africa.

Boswell, Rosabelle. 2008. Scents of identity: Fragrance as heritage in Zanzibar katika *Journal of Contemporary African Studies* 20,3: 295-311.

Carlisle, Janice. 2001. The Smell of Class: British Novels of the 1860s. *Victorian Literature and Culture* 29,1: 1-19.

Chiraghdin, Shihabdin. 1987. *Malenga wa Karne Moja.* Nairobi: Longman

Chum, Haji. 1994. *Msamiati wa Pekee wa Kikae Kae Specific Vocabulary*. Uppsala: Nordic Association of African *Studies*.

Eisenberg, Andrew. 2017. The Swahili Art of Indian Taarab: A Poetics of Vocality and Ethnicity on the Kenyan Coast. *Comparative Studies of South Asia, Africa and the Middle East.* 37,2: 336-354 • DOI 10.1215/1089201x-4133978.

Holly, Dugan. 2011. *The Ephemeral History of Perfume: Scent and Sense in Early Modern England.* Baltimore: The Johns Hopkins University Press.

Hourani, Goerge. 1951. *Arab Seafaring in the Indian Ocean in Ancient and Early Medieval Times.* Princeton, NJ: Princeton University Press

Hugo, Victor. 2000. *Les Orientales / Les Feuilles d'automne*. *Introduced and annotated by Franck Laurent*. Paris: Librairie Générale Française.

Khamis, Amour. 2008. *Jadi na Utamaduni wa Maswahili wa Zanzibar*. Zanzibar: BAKIZA.

Kipacha, Ahmad. 2015. The Blason Populaire in Swahili Paremia, *Provebium* 32: 205-220.

Knappert, John. 1970. *Myths and Legends of the Swahili*. London: Heinemann.

Knappert, John. 1979. *Four Centuries of Swahili Verse*. Nairobi: Heinemann.

Kresse, Kai 2009. Knowledge and Intellectual Practice in a Swahili Context: ‘Wisdom and the Socail Dimensions of Knowledge. *Africa* 79,1: 148-167.

Lodhi, Abdulaziz. 2000. *Oriental Influences in Swahili. A Study in Language and Culture Contacts*. Orientalia et Africana Gothoburgensis 15. Göteborg: Acta Universitatis Gothoburgensis.

Manalansan, Martin. 2006. Immigrant Lives and the Politics of Olfaction in the Global City. Jim Drobnick (ed.) *The Smell Culture Reader*, New York: Berg. 41-52.

Maxwell, Catherine. 2017. *Scents and Sensibility: Perfume in Victorian Literary Culture*. Oxford: Oxford University Press.

McHugh, James. 2011. The incense trees of the land of emeralds: The exotic material culture of Kāmaśāstra. *Journal of Indian Philosophy* 39,1: 63-100.

Mdungi, Abbas. 2009. *Arudhi ya Ushairi wa Kiswahili*. Zanzibar: Al Mafazy.

Miehe, Gutrin., A. Abdalla, Ahmad N. J. Bhalo, A. Nabahany, A. Baschiera, C. Dittemer, F. Topan, Mohamed A. Abdulaziz, Said A. Khamis, Yahya A. Omar, and Zeina M. F. Al-Bakary. 2007. *Liyongo Songs. Poems attributed to Fumo Liyongo.* Köln: Rüdiger Köppe Verlag.

Mnyampala, Mathias. 2014. *Waadhi wa Ushairi.* Dar es Salaam: TATAKI.

Mulokozi, Mugyabuso. 1982. Protest and Resistance in Swahili Poetry 1600-1885. *Kiswahili*, 49,1: 25-54.

Mulokozi, Mugyabuso (Mh.). 1999. *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.

Nasir, Sayyid Abdallah. 1972. *Al-Inkishafi.* Oxford: Oxford University Press (Imefasiriwana kuhaririwa na Hichens, William).

Nicolini, Beatrice. 2003. The Western Indian Ocean as Cultural Corridor: Makran, Oman and Zanzibar through Nineteenth Century European Accounts and Reports. *Middle East Studies Association Bulletin* 37,1: 20-49

Nigel, Groom. 1981. *Frankincece and Myrrh: A Study of the Arabian Incence Trade*. London: Intenrational book center.

Njozi, Hamza. 1990. Utendi wa Mwanakupona and Reception Aesthetics. *Kiswahili* 57: 55-67.

Nyamaume, Khamis. 2004. *Diwani ya Ustadh Nyamaume*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Pera, Ridhiwani. 1996. Shairi la Fumo Lyongo MS 57. *Kiswahili* 59: 23-32.

Popova, Yanna. 2003. 'The fool sees with his nose:' metaphoric mappings in the sense of smell in Patrick Süskind's Perfume. *Language and Literature: International Journal of Stylistics* 12,2: 135-151.

Rettová, Alena. 2010. Philosophy in Utenzi Metre. Expressions of Ideas and values in Post-Independence Swahili Historiographic Poetry and the Mediality of African Philosophy, *Swahili Forum* 17: 34-57.

Rimmel, Eugene. 1865. *Book of Perfumes*, London: Chapman and Hall.

Robert, Shaaban. 1958. *Mapenzi Bora.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Robert, Shaaban. 1972. *Almasi za Afrika.* London: Thomas Nelson and Sons Ltd.

Senkoro, Fikeni. 1988. *Ushairi : Nadharia na Tahakiki.* Dar es Salaam: DUP.

Shafi, Adam. 1999. *Vuta N'kuvute*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Taib Ali, Abdulrahim. 2016. Usawiri wa Mwananmke katika Nyimbo za Harusi: Visiwani Zanzibar. *Jahazi* 1: 63.83

Timammy Raya & Swaleh Amir. 2013. A thematic analysis of Utendi wa Mwanakupona: a Swahili /Islamic persective. *International Journal for Innovation Education and Research* 1,3: 60-72.

Vierke, Clarrisa. 2016. From across the ocean: considering travelling literary figurations as part of Swahili Intellectual history. *Journal of African Cultural Studies* 28, 2: 225-240.

Wamitila, Kyallo. 2004. *Kamusi ya Tashbiha, Vitendawili, Milio na Mishangao*. Longhorn Publishers: Nairobi.

Yahaya-Othman Saida & Yahaya, Abdulhakim (wah) (2004). *Howani Mwana Howani: Tenzi za Zaynab Himidi Mohammed*. Dar es Salaam: TUKI.